Jarida la Wizara ya Afya

# Afya Habari

JARIDA LA MTANDAONI LA WIZARA YA AFYA | TOLEO, NO. 16, FEBRUARI 2024






# TUNABORESHA AFYA

MTU NI AFYA, JALI AFYA YAKO





## BODI YA UHARIRI

**MWENYEKITI**
Dkt. John Jingu
KATIBU MKUU

**MHARIRI**
Englibert Kayombo

**MHARIRI MSAIDIZI**
Emmanuel Malegi

**WAJUMBE**
Englibert Kayombo
Emmanuel Malegi
Majid Abdulkarim
Said Nyaoza
Hassan Kimweri
Shaban Juma
Cletus Sanga
Abdulwaheed Madenge
Aisha Swahibu

**WASANIFU**
Englibert Kayombo
Said Nyaoza

@wizara_Afyatz
www.moh.go.tz


# YALIYOMO


Rais Samia atoa bilioni 1 kugharamia watoto 20 wa Selimundu....UK 2







Serikali kuimarisha kinga na tiba ya maradhi ya saratani nchini .... UK 3

Tanzania yajadili namna ya ununuzi wa dawa adimu kutoka Cuba .... UK 4







Serikali yatumia bilioni 346.4 kutibu wagonjwa wa Kisukari na Tezi Dume.... UK 5

Wagonjwa wa moyo zaidi ya 800 wafanyiwa upasuaji mkubwa.... UK 6








Waganga wafawidhi watakiwa kusimamia matumizi ya lugha za staha katika vituo vya kutolea huduma .... UK 6

Wataalam wa afya ngazi ya msingi wakumbushwa uwajibikaji kazini..... UK 7




Ugonjwa wa Kifafa unaongoza Duniani katika magonjwa ya mishipa ya fahamu .... UK 8





Watanzania watakiwa kuzingatia mtindo bora wa maisha ili kuepuka magonjwa yasiyoambukiza .... UK 9

Wazazi waaswa kuwapeleka watoto wao kupata chanjo ya surua na rubela.... UK 10






Kamati ya Bunge yaridhishwa na utendaji wa MSD... UK 11

Waratibu wa afya watakiwa kuhakikisha fedha za Chanjo na Lishe zinafika zinapokusudiwa kwa wakati.... UK 12





Simamieni usafi katika maeneo yenu (kipindupindu kinaletwa na uchafu) .... UK 13

Maambukizi ya vvu yamepungua kutoka 7% mwaka 2003/2004 hadi 4.4% mwaka 2022/2023 kwa tanzania..... 14





Watumishi sekta ya afya wasisitizwa mahusiano mazuri kazini ili kutoa huduma bora kwa wananchi .... UK 15




MOI yapokea msaada wa mtambo wa upasuaji wenye thamani ya tsh milioni 500. .... UK 16

BMH yapokea magari ya kubebea wagonjwa .... UK 17





Tanzania mfano mapambano ya kupnguza vifo vitokanavyo na uzazi..... UK 18

Waganga wafawidhi mkasimamie huduma bora kwa wananchi - Waziri Ummy..... UK 19





Serikali yabainisha vipaumbele 6 vya kisera katika sekta ya afya 2024/25 .... UK 20

Badilisheni mtindo wa maisha - Prof. Janabi ..... UK 21






Serikali inatambua mchango wa sekta binafsi katika kuwahudumia wananchi .... UK 22



# Rais Samia atoa bilioni 1 kugharamia watoto 20 wa Selimundu

**Na. Englibert Kayombo**
**DODOMA**

Waziri wa Afya, Mhe. Ummy Mwalimu, amesema katika kuendelea kuboresha huduma za afya nchini Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa fedha zenye thamani ya shilingi bilioni 1 kwa ajili ya kutibu watoto 20 wenye ugonjwa wa Selimundu (Sickle Cell) mpaka kufikia Juni 2024.

Waziri Ummy amesema hayo  Februari 1, 2024 wakati wa ziara ya Rais Samia katika Hospitali ya Benjamin Mkapa jijini Dodoma, ambapo aliwajulia hali watoto waliopandikizwa uroto katika Hospitali hiyo.

"Hatua hii inaonyesha dhamira ya serikali katika kuboresha huduma za afya na kuhakikisha upatikanaji wa matibabu kwa watu wenye magonjwa maalum kama ugonjwa wa Selimundu ambapo hadi kufikia sasa jumla ya watoto watatu wameshapandikizwa uroto". Amesema Waziri Ummy.

Waziri Ummy ameongeza kuwa jitihada za Serikali katika kusaidia makundi yenye mahitaji maalum katika jamii zinaonesha azma thabiti ya kuimarisha huduma za afya na ustawi wa wananchi kwa kutoa fedha kwa ajili ya matibabu ya wagonjwa mbalimbali ambapo Serikali inaonyesha kujali na kuthamini maisha ya raia wake, hasa wale walio katika mazingira magumu ya kiafya.

Aidha, ameongeza kuwa hatua hiyo inatoa ishara ya uongozi mathubuti wa Rais Samia wa kujali na kuwajibika, ambao unazingatia mahitaji ya wananchi wake.

"Rais Samia amewezesha upatikanaji wa huduma bora za afya ikiwa ni moja ya vipaumbele vya Serikali yake katika kuleta maendeleo endelevu na ustawi wa jamii". Amesema Waziri Ummy.



# Serikali kuimarisha kinga na tiba ya maradhi ya saratani nchini

**Na. Hassan Kimweri**
**DAR ES SAlAAM**

Serikali imesema itaendelea kuboresha na kujenga miundombinu ya vituo vya afya pamoja na kuweka mikakati inayolenga kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wote ili kuimarisha kinga na Tiba ya Maradhi ya Saratani

Hayo yameelezwa na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi Februari 06, 2024 jijini Dar es Salaam wakati wa kikao cha uwekezaji na wadau wa maende kwa ajili ya uanzishwaji wa Kituo cha Umahiri wa Matibabu ya Saratani nchini Tanzania. Kituo ambacho kitakuwa pekee cha umahiri wa matibabu ya Saratani katika nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara.

"Maradhi ya Saratani ni ugonjwa unaoathiri mamilioni ya watu kote ulimwenguni, hivyo kama jamii tunapaswa na sisi kuwekeza katika kinga na tiba ya maradhi haya, tayari Serikali imeanza kuchukua hatua na tunashuhudia hatua katika ujenzi wa miundombinu ya huduma za afya na mikakati inayolenga kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za matibabu kwa wote" amesema Dkt. Mwinyi.

Dkt. Mwinyi ameongeza kuwa uwekezaji katika huduma za Saratani nchini unakusudia kujenga matumaini ya maisha kwa watu na familia ambazo zimekubwa na changamoto hiyo.

"Lengo la Serikali ni kuhakikisha kila mtu anaekutana na changamoto ya Saratani anapata huduma kamili na matibabu stahiki, Maono ya Mhe. Rais Dkt Samia yanalenga mbali na kuzingatia maendeleo endelevu ikiwemo matumizi ya nishati mbadala kukuza uhifadhi wa mazingira na kuhakikisha matumizi sahihi ya rasilimali zetu za asili, malengo haya yanaonesha dhamira ya dhati ya kutunza mazingira kwa ajili ya kizazi cha sasa na cha baadae, juhudi hizi ni sehemu ya Mkakati wa kukabiliana na ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo saratani" amesema Dkt. Mwinyi.

Aidha Rais. Dkt. Mwinyi akatumia fursa hiyo kuhimiza juu ya umuhimu wa ushirikiano utakaosaidia kutimiza malengo ya nchi na kuhakikisha upatikanaji wa matibabu bora kwa wagonjwa wa Saratani.

"Kwa kupitia ushirikiano kati ya Serikali, sekta binafsi, watafiti na wataalam wa tiba tunaweza kubadilisha kabisa taswira ya huduma za saratani, tuwe na dhamira ya dhati ya kufanya kazi bila kuchoka katika kukabiliana na ugonjwa wa Saratani ili kuleta matumaini kwa wale watakaopata changamoto hio ya kiafya"





# Tanzania yajadili namna ya ununuzi wa dawa adimu kutoka Cuba

**Na. Aisha Swahibu**
**DODOMA**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu akiwa na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Grace Magembe pamoja na Wakurugenzi wa Wizara ya Afya Februari 2, 2024 wamekutana na Balozi wa Tanzania nchini Cuba Bw. Humphrey Polepole, wadau wa Hospitali, MSD pamoja na Mamlaka ya Dawa na Vifaa tiba (TMDA) ambapo wamefanya mazungumzo katika ofisi za Wizara ya Afya Mkoani Dodoma.

Mazungumzo hayo yamelenga kuona namna gani Serikali ya Tanzania inaweza kuanzisha ushirikiano wa ununuzi wa dawa adimu moja kwa moja kutoka katika viwanda vya dawa vya nchini Cuba.

Balozi Polepole amesema hivi sasa Tanzania na ukanda wa nchi za SADC kuna uhaba wa dawa za kutibu magonjwa kama vidonda vitokanavyo na Kisukari, baridi yabisi pamoja na dawa za kutibu ugonjwa wa Vitirigo.

“Dawa hizi zinazalishwa nchini Cuba na kiwanda cha Biocube Pharma ambazo zimeonesha matokeo makubwa, hivi sasa wagonjwa wa Kisukari wenye vidonda ambavyo haviponi, nchini Cuba hawakatwi tena viungo kutokana na madhara yanayosababishwa na vidonda hivyo bali hutumia dawa hizo na kupona kabisa.” Amesema Bw. Polepole

Aidha, Balozi Polepole ameongeza kuwa kiwanda hicho kinazalisha dawa za kutibu ugonjwa wa vitirigo (mabaka meupe katika mwili) pamoja na baridi yabisi na imeonekana na kuna uhitaji mkubwa wa dawa hizo nchini na ukanda wa nchi za SADC kwani kuna wananchi wengi wanasumbuliwa na maradhi hayo.

Kwa upande wake, Waziri Ummy amemshukuru Balozi Humphrey Polepole kwa weledi wake wa utendaji akiwa kama Balozi nchini Cuba kwa kutafuta fursa ambazo zitaisaidia Serikali kupunguza gharama za matibabu kwa watu wenye matatizo hayo.

“Sasa hivi Serikali inatumia gharama kubwa kwa matibabu ya watu wenye vidonda vitokanavyo na Kisukari, Baridi Yabisi pamoja na Vitirigo ambapo takwimu zinaonesha Hospitali ya Taifa Muhimbili pekee imetumia Shilingi bilioni 1.4 katika matibabu.” Amesema Waziri Ummy

Mwisho, Waziri Ummy Mwalimu amemhakikishia Balozi Polepole kuwa Serikali kupitia Wizara ya Afya itaanza mchakato mara moja wa kununua dawa hizo ili ziwe mkombozi kwa watu wenye matatizo hayo hasa vidonda vitokanavyo na Kisukari ambavyo haviponi na wengi wao huishia kukatwa viungo

# Serikali yatumia bilioni 346.4 kutibu wagonjwa wa Kisukari na Tezi Dume

**Na. Majid Abdulkarim**
**DODOMA**

Serikali imesema kuwa gharama ya kutibu wagonjwa wa Sukari kwa mwaka ni shilingi bilioni 300, na gharama za kutibu wagonjwa wote wa tezi dume ni shilingi bilioni 46.42 hivyo kupelekea jumla ya gharama za matibabu kwa magonjwa haya mawili kufikia shilingi bilioni 346.42.

Kauli hiyo imetolewa na Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel  Bungeni Jijini Dodoma wakati akijibu swali namba 98 kwa niaba ya Waziri wa Afya, Mhe. Ummy Mwalimu ambapo swali hilo limeulizwa na Mbunge wa Igalula, Mhe. Venant Daud aliyeuliza Je, Serikali haioni haja ya kutoa msamaha wa matibabu kwa wagonjwa wa sukari na tezi dume nchini.

Dkt. Mollel ameeleza kuwa gharama za matibabu ya magonjwa hayo mawili ni kubwa sana wakati bajeti ya dawa Ina vifaa tiba kwa mwaka ni shilingi bilioni 200.

"Ikitokea huduma ya matibabu kwa magonjwa haya mawili kutolewa bure kutasababisha huduma nyingine katika nchi kusimama". Amesema Dkt. Mollel.

Aidha, amesema Serikali inasisitiza utekelezaji wa Sera ya Afya ya Mwaka 2007 ya kutoa huduma ya Msamaha kwa wananchi wasio na uwezo wa kulipia huduma za afya hata hivyo wenye uwezo wa kulipia wataendelea kuchangia.

Dkt. Mollel ameongeza kuwa mwaka 2022/2023 gharama ya msamaha wa matibabu kwa wagonjwa wa sukari na saratani ya tezi dume ilikuwa kiasi cha shilingi bilioni 70.4

Vile vile Dkt. Mollel amesisitiza viongozi wa Mamlaka za mikoa na Serikali za mitaa kusimamia sekta ya afya kikamilifu ili kuleta ubora wa huduma ili kutekelza azma ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kila Mtanzania kupata huduma bora za afya.



# Wagonjwa wa moyo zaidi ya 800 wafanyiwa upasuaji mkubwa




**Na. Cletus Sanga**
**ZANZIBAR**

Wagonjwa wa moyo zaidi ya 800 wamefanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo huku wengine zaidi ya 2,000 kufanyiwa upasuaji wa tundu dogo kwa kutumia mtambo wa 'cath-lab' kwa kipindi cha miaka Miwili katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI).

Hayo yamesemwa Februari 9, 2024 na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Isdor Mpango wakati akifungua mkutano wa Kimataifa wa magonjwa ya moyo mjini Zanzibar.

"Lakini pia, wagonjwa wa moyo zaidi ya laki mbili wamepatiwa matibabu katika Taasisi hiyo kwa kipindi cha miaka miwili ambapo kati yao wagonjwa 2,400 walitoka nchi za jirani za Comoro, Congo DRC, Kenya, Malawi, Mozambique, Rwanda, Uganda pamoja na Zambia." Amesema Dkt. Mpango

Amesema, kutokana na huduma zinazotolewa na Taasisi hiyo zimeweza kuifanya JKCI kuwa Taasisi ya umma inayoongoza katika kutoa huduma za matibabu ya moyo Afrika Mashariki na kati hivyo kuwavutia wanataaluma kutoka nchi za jirani zikiwemo nchi za Malawi, Zambia na Rwanda kujenga mashirikiano.

Aidha, Mheshikiwa Makamu wa Rais Dkt. Mpango amesema kupitia Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete Serikali imeweza kuokoa Tsh: Bilioni 63 fedha za Kitanzania zilizokuwa zinatumika kwa ajili ya matibabu ya moyo nje ya nchi.

"Kati ya mafanikio yaliyofanywa na Taasisi hiyo ni pamoja na uanzishwaji wa kambi maalumu ya matibabu ya moyo ijulikanayo kwa jina la Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan services ambayo imekuwa ikitoa huduma ya kuwajengea uwezo wataalamu wa Afya waliopo katika hospitali za mikoa na kuwafikishia karibu huduma za matibabu ya moyo wananchi wanaohitaji matibabu hayo." Amesema Dkt. Mpango

Pia amesema, Serikali itaendelea kuwekeza kakika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete kwa kupanua huduma za matibabu na kumtaka Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu kufuatilia gharama za ujenzi utakaofanyika JKCI Dar Group na kuziwasilisha Serikalini mapema ili serikali iweze kuwekeza katika ujenzi huo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) Dkt. Peter Kisenge amesema JKCI imeanzisha mkutano huo wa kisayansi kwa wataalamu wa Afya nchini ukiwa na lengo la kuwapa ujuzi wataalamu wa afya nchini kuhusu magonjwa ya moyo.

"Mkutano wetu unahusisha huduma za awali kabisa ambazo mgonjwa wa moyo anatakiwa kupata lengo likiwa kuokoa maisha ya wagonjwa wa moyo kwani wengi wao hufika JKCI kwa kuchelewa." Amesema Dkt. Kisenge




# Waganga wafawidhi watakiwa kusimamia matumizi ya lugha za staha katika vituo vya kutolea huduma

**Na. Abdulwaheed Madenge**
**DODOMA**

Katibu Mkuu wa wizara ya Afya Dkt John Jingu amewataka Waganga wafawidhi wa vituo vya kutolea huduma za afya kuhakikisha wanasimamia na kuimarisha mawasiliano baina ya mtoa huduma na mpewa huduma kwa kuzingatia matumizi ya lugha zenye staha.

Dkt. Jingu ameyasema hayo  Februari 14, 2024 Jijini Dodoma wakati wa mkutano wa mwaka wa waganga wafawidhi wa vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya msingi, ambapo amesisitiza wapo baadhi ya watoa huduma wanaharibu taaluma hiyo kutokana na kukosa namna sahihi za kuwa wakarimu kwa wagonjwa jambo linalopekea Manung'uniko makubwa katika jamii.

"Baadhi yetu, kunachangamoto kubwa ya lugha wanazozitumia wakati wa kutoa huduma kwa wahudumiwa si za staha na hii inaleta malalamiko, wakati mwingine tunalazimka kuunda timu, tunapoteza rasilimali baada ya kupeleka fedha katika kuboresha huduma tunaanza kuchunguzana, lugha ya staha ni muhimu ukizingatia tunaowahudumia ni wagonjwa ni watu wenye shida." amesema Dkt. Jingu.

Pia Dkt. Jingu amelaani vitendo vya baadhi ya watoa huduma za afya nchini kuendekeza matumizi ya simu hasa wawapo katika maeneo ya kazi.

"Hili ni jipya halikuwepo zamani, Unakuta Mgonjwa yupo pale badala ya kumuhudumia mhudumu yupo busy na simu na mgonjwa anaweza pata madhara ambayo kama ungekuwa makini akili yako isingekuwa kwenye simu ungeweza kumsaidia, kwahiyo hili ni jambo ambayo ni lazima tulidhibiti wakati wa kutoa huduma." Amesema Dkt. Jingu

Aidha Dkt. Jingu amesisitiza kurekebishana kimaadili na uadilifu kwa baadhi ya watoa huduma hasa kudhibiti matumizi mabaya ya miundombinu ya vituo vya afya pamoja na kudhibiti wizi wa Dawa.

"Sisi wote tunaapa kabla ya kuruhusiwa kufanya majukumu yetu, twendeni tukaishi viapo vyetu, na mjue kwamba nyie ndio sekta, tuna mawaziri wetu na sisi wasaidizi wao lakini sekta hasa ni ninyi, 99% ya sekta inapatikana kwenu nyie, twendeni tukailinde sekta yetu watu wapate huduma bora, nyie wote ni wawakilishi wa serikali katika sekta ya Afya bila kujali umiliki ni wanani" amesema Dkt. Jingu

# Wataalam wa afya ngazi ya msingi wakumbushwa uwajibikaji kazini

**Na. Shaban Juma**
**DODOMA**

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. Grace Magembe amewataka Madaktari, Wauguzi, Wataalamu wa maabara na Wataalamu wote wa afya kuwa na utaratibu wa kupita maeneo ya huduma kuangalia wananchi wanavyopata huduma ikiwemo kuangalia muda wanaokaa na kusubiri kupata huduma badala ya kukaa ofisini.

Dkt. Magembe ametoa maelekezo hayo Jijini Dodoma wakati akizungumza na Waganga wafawidhi kabla ya ufunguzi wa Mkutano wa kwanza wa mwaka kwa waganga wafawidhi wa vituo vya kutolea huduma za Afya ya msingi nchini.

"Nasisitiza daktari, muuguzi, mtaalamu wa maabara na wengine wote piteni mawodini na kufungua majalada ya wagonjwa kuona huduma gani wagonjwa wamepatiwa tangu wamefika hospitali, je wanapata dawa na vipimo vilivyoandikwa, watumishi wapo na kama wanawajibika". Amesisitiza Dkt. Magembe.

Ameongeza kwa kusema kuwa watumishi wasijifungie maofisini tu, bali watumie ujuzi wao kama viongozi wa vituo kuhakikisha wanatoa Huduma bora kwa wananchi ili kuleta thamani ya uwekezaji wa Rais Samia Suluhu Hassan katika sekta ya afya nchini.

"Kama wananchi watafika mahali hawaoni tofauti ya ukiwepo na usiwepo basi wewe kitaaluma ni mfu maana taaluma yako haigusi maisha ya watu". Amesema Dkt. Magembe.
Hata hivyo amewataka waganga hao kuimarisha ushirikiano wao na watumishi wanao waongoza ili kuleta ubora wa huduma katika kuwahudumia wananchi.

Aidha, Mkutano huo ulenga kuboresha uwajibikaji katika kutoa huduma bora za Afya ya msingi kwa Watanzania ili kila mwananchi anufaike na uwekezaji uliofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan katika Sekta ya Afya nchini.

Mkutano huo umebebwa na kaulimbiu "Uwajibikaji ni nguzo muhimu katika utoaji wa huduma bora za Afya ya msingi"





# Ugonjwa wa Kifafa unaongoza Duniani katika magonjwa ya mishipa ya fahamu

**Na. Said Nyaoza**
**DODOMA**

Inakadiriwa kuwa takribani watu milioni 50 duniani wana ugonjwa wa kifafa na wengine wapya milioni sita wanagundulika kila mwaka ambapo nchini Tanzania kuna wagonjwa zaidi ya milioni moja wanaokabiliwa na tatizo hilo.

Hayo yameelezwa na Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Joseph Nagu wakati akizungumza kwenye kongamano la maadhimisho ya siku ya kifafa duniani lililoandaliwa na Chama cha Watalam wa Kifafa Tanzania (TEA) na kuadhimishwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili ambapo ameitaka jamii kuacha tabia ya kuwaficha wagonjwa wenye kifafa kwakuwa wagonjwa hawa wakitumia dawa wanaweza kuishi kama watu wengine.

Ameongeza kuwa pamoja na kwamba ugonjwa huu umeanza siku nyingi bado jamii inaendelea kuhusisha na imani potofu na kuwaficha watoto wenye ugonjwa huo ndani na kuwasababisha kukosa huduma za matibabu mapema.

"Mtu mwenye ugonjwa wakifafa akichelewa kupata matibabu anaweza kupoteza maisha mapema kutoka na madhara mbalimbali ikiwemo kudondoka sehemu zenye hatari ikiwemo kwenye moto au kugongwa na gari" amesemea Prof. Nagu.

Pamoja na hayo amesema kuwa Serikali kupitia Wizara ya Afya inaendelea kuongeza vituo vya kutolea huduma na kuweka dawa muhimu ili kupunguza uwezekano wa mtoto anayezaliwa kupata ugonjwa wa kifafa.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa TEA, Prof. William Matuja amesema kuwa ugonjwa wa kifafa unasababishwa na magonjwa yanayoshambulia ubongo hasa wakati mtoto anapozaliwa, mtoto kupata ugonjwa wa degedege unaojirudia, malaria kupanda kichwani au kula vyakula vyenye vijidudu.
Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji Hospitali ya Taifa Muhimbili, Prof. Mohamed Janabi amesema kwa sasa kuna mabadiliko katika matibabu hivyo ni vyema wataalam kwenda sambamba na mabadilko hayo, pia amewataka kutumia kongamano hilo kujadili na kubadilishana uzoefu hasa katika maswala ya tiba.

# Watanzania watakiwa kuzingatia mtindo bora wa maisha ili kuepuka magonjwa yasiyoambukiza



**Na. Hassan Kimweri**
**ZANZIBAR**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu ameendelea kuwasisitiza wananchi kuzingatia mtindo bora wa maisha ili kuepuka magonjwa Yasiyoambukiza kwa kuwa takwimu za 2012 zinaonesha Watanzania 9 kati ya 100 wana Kisukari huku Watanzania 26 kati ya 100 wana Shinikizo la Juu la damu (Presha).

Waziri Ummy amesema hayo Februari 9, 2024 kwenye ufunguzi wa Kongamano la Kimataifa la 'Heart Team Africa' lililofunguliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Isdor Mpango Mjini Zanzibar.

"Kulingana na Utafiti wa STEPs wa WHO za Mwaka 2012 (tunaposubiri data za 2022 kutolewa hivi karibuni) zineonesha kuwa Watanzania 9 kati ya 100 wana Kisukari huku Watanzania 26 kati ya 100 wana Shinikizo la Juu la damu ." Amesema Waziri Ummy

Amesema, katika vitu vya kuzingatia ni pamoja na kupunguza matumizi ya sukari, chumvi, mafuta kidogo, kuacha matumizi ya tumbaku, unywaji pombe uliopitiliza, kuongeza kasi ya mazoezi ya mara kwa mara ikiwemo mazoezi ya viungo.

Aidha, Waziri Ummy amesema Serikali itaendelea kuwekeza kwa kuboresha matibabu ya moyo nchini na upande wa majengo, kuwa na Vifaa Tiba vya kisasa vinavyofanana na vilivyopo nchi zilizoendelea pamoja na kuwaendeleza wataalamu wa moyo kuwa mabingwa wabobezi.

"Serikali imetupa fedha kiasi cha Tsh: Bilioni 9 kwaajili ya kusomesha madaktari kuwa mabingwa wabobezi katika masuala ya moyo na hii itahusisha wataalamu wa Afya ambao ni madaktari wa upasuaji, wauguzi, wafamasia, na madaktari wa usingizi." Amesema Waziri Ummy

Pia, Waziri Ummy amesema Serikali chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imepata mafanikio makubwa katika Sekta ya Afya, hivyo inaendelea na juhudi za kuokoa maisha ya Watanzania wenye magonjwa Yasyoambukiza ikiwemo kutoa matibabu na elimu.

"Tunaona fahari kubwa kwa yote ambayo tumefanikiwa katika vituo vyetu vya huduma za Afya ikiwemo kutoa huduma ya hali ya juu nchini Tanzania kama vile Upandikizaji wa Valve ya mishipa kwenye taasisi ya JKCI, Upasuaji wa 'Transcatheter' kwa kutumia Angio Suite katika Taasisi yetu ya Kitaifa ya Mifupa." Amesema Waziri Ummy

Mkutano huo umeangaziwa na mada mbalimbali ambazo zitajadiliwa hapo ni pamoja na namna ya Uchunguzi wa upigaji picha, Upasuaji wa Mishipa, Urekebishaji wa viungo, Uuguzi na Kinga ambapo majadiliano hayo muhimu yatapelekea kubadilishana uzoefu kati ya wajumbe wote waliyopo.



# Wazazi waaswa kuwapeleka watoto wao kupata chanjo ya surua na rubela

**Na. Aisha Swahibu**
**DAR ES SALAAM**

Serikali kupitia Wizara ya Afya Nchini imewataka Wazazi, Walezi na Walimu kujitokeza kwa wingi kuwatoa watoto wote kwenye kampeni kubwa ya kupata chanjo ya Magonjwa ya Surua na Rubela ambayo itaanza mwezi wa pili ili kuimarisha kinga zao katika kuepukana na magonjwa ya milipuko.

Akizungumza Februari 01, 2024 Jijini Dar es Salaam Wakati wa Ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kutathimini Huduma za Chanjo Nchini kwa mwaka 2023, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dkt. Grace Magembe amewahimiza wananchi kufanya usafi wa mazingira ili kuendelea kuepukana na magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu.

"Ni jukumu la wananchi kujikinga na maradhi ya milipuko kwa kufanya usafi wa mazingira, kunawa mikono ili kuhakikisha wanapoanda chakula katika mazingira bora hasa wakati wa kuwapatia watoto chakula na wazingatie kanuni za Afya" amesema Dkt. Magembe

Aidha, Dkt. Magembe amesema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa ya kununua vifaa vya afya, hivyo watumishi wanatakiwa kuzingatia maadili katika kuwapa wananchi taarifa sahihi, lengo ni kuhakikisha kwamba wananchi wanahudumiwa vizuri pindi wanapopata changamoto zao kutatuliwa kwa haraka.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu amesema takribani mikoa nane tayari ina maambukizi ya kipindupindu, hivyo amewataka waganga wakuu wa mikoa kusimamia afua za usafi ili kuhakikisha miundombinu ya kunawia mikono ipo katika kukabiliana na magonjwa.

# Kamati ya Bunge yaridhishwa na utendaji wa MSD

**Na. Emmanuel Malegi**
**DODOMA**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Maswala ya UKIMWI imeitaka Bohari ya Dawa (MSD) kuongeza ufanisi, ubunifu wa hali ya juu kwa kuhakikisha dawa zinanunuliwa, zinahifadhiwa sehemu sahihi, kusambaza dawa hizo kwa wakati katika sehemu zenye uhitaji na kukusanya madeni ili kuweza kuwa imara na taasisi endelevu.

Wito huo umetolewa Jijini Dodoma na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Afya na Maswala ya UKIMWI, Mhe. Stansilaus Nyongo baada ya kupokea taarifa ya hali ya utendaji na majukumu ya Bohari ya Dawa (MSD).

Mhe. Nyongo amesema kuwa wao kama wawakilishi wa wananchi wataendelea kuishinikiza serikali kuiwezesha MSD kupata mtaji ili kujiendesha kiufanisi katika kusambaza dawa kwa wakati.

“Bohari kuu ina majukumu ya kununua, kutengeneza, kuhifadhi dawa pamoja na kusambaza dawa katika vituo vya vyote nchini”. Ameeleza Mhe. Nyongo.

Mhe. Nyongo amesema kwa ujumla kamati imeridhishwa na hali ya utendaji wa Bohari ya Dawa na mipango yake ya utekelezaji wa majukumu yake ikiwemo uzalishaji wa dawa ili kupunguza kununua dawa nje ya nchi.

Kwa upande wake Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amempongeza Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Mavele Tukai kwa uongozi imara katika taasisi hiyo na kufanya upatikanaji wa dawa kwa wakati kuongezeka nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Mavele Tukai amesema MSD ina mipango ya kuanzisha kampuni tanzu ambayo itaingia mikataba na makampuni binafsi ya ndani na nje katika kuwekeza viwanda vya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali za dawa na vifaa tiba nchini.



# Waratibu wa afya watakiwa kuhakikisha fedha za Chanjo na Lishe zinafika zinapokusudiwa kwa wakati




**Na. Said Nyaoza**
**DAR ES SALAAM**

Waratibu wa Afya ngazi zote wametakiwa kuhakikisha wanasimamia fedha za chanjo na lishe zinazotolewa na Wadau pamoja na Serikali zinafika zinapokusudiwa kwa wakati ili kupunguza tatizo la Ukosefu wa elimu ya lishe na magonjwa ya mlipuko.

Hayo yamesemwa na Naibu katibu Mkuu OR-Tamisemi anayeshughulikia Afya Dkt. Wilson Charles Februari 3, 2024 jijini Dar es Salam Wakati akifunga Mkutano mkuu wa mwaka wa tathimini ya huduma za chanjo nchini kwa mwaka 2023 ambapo amewasihi Wasimamizi kutosita kuwachukulia hatua ama kuwawajibisha wale wote watakao bainika kufuja fedha hizo.

“Ushirikiano hafifu, kukosa mipango na mikaka pamoja na matumizi mabaya ya fedha vimekua changamoto ya kukwamisha huduma bora za lishe na chanjo, Tumekuwa tukipokea fedha kutoka shirika la GAVI kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Chanjo.

Hata hivyo suala hili halijapewa kipaumbele, hivyo niwakumbushe tena kila Mkoa ukusanye nyaraka hizo na kuziwasilisha OR-TAMISEMI kabla ya tarehe 15 Februari 2024 kwa ajili ya hatua nyingine” amesema Dkt. Charles.

Dkt. Charles ameongeza kuwa kila Mkoa ni vema uimarishe ufuatiliaji na tathmini za utekelezaji wa Mkakati wa Kumfikia Mtoto kwa Chanjo (Reach Every Child) katika ngazi ya vituo vyetu vya huduma za Afya.

“Mikoa na Halmashauri ziimarishe usimamizi na kutoa msaada wa kiufundi kwenye vituo vya huduma ili kuinua kiwango cha ubora wa huduma zinazotolewa. OR-TAMISEMI kwa kushirkiana na Wizara ya Afya itaendelea kutafuta rasilimali kadiri fursa zinavyopatikana na kuzielekeza rasilimali hizo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kuimarisha huduma za Afya Msingi ikiwemo Chanjo,” amesema Dkt. Charles.

Kuelekea utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Chanjo ya Surua na Rubella inayotarajiwa kuanza tarehe 15 hadi 18 Februari, 2024, Dkt. Charles amesisistiza wasimamizi wa kampeni hio kuhakikisha Watoto wote wanafikiwa pamoja fedha zilizotengwa kwa shughuli hiyo zinatumika vizuri.



# Maambukizi ya VVU yamepungua kutoka 7% mwaka 2003/2004 hadi 4.4% mwaka 2022/2023 kwa Tanzania

**Na. Hassan Kimweri**
**DAR ES SALAAM**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amesema kwa Tanzania maambukizi ya VVU yamepungua kutoka asilimia 7 mwaka 2003/2004 hadi kufikia asilimia 4..4 mwaka 2022/2023, kukiwa na tofauti kati ya watu na maeneo mbalimbali ya kijiografia.

Waziri Ummy amesema hayo Februari 6, 2024, jijini Dar es Salaam wakati akifungua mkutano wa siku Mbili wa mapitio ya kimkakati wa PEPFAR COP muhula wa 23 kwa lengo la kutathmini hatua iliyofikiwa kuhusu mwitikio wa VVU katika kufikia udhibiti wa UKIMWI ifikapo mwaka 2030.

“kikao hiki kinalenga kujadili na kubainisha mikakati itakayowezesha ufanisi wakati wa utekelezaji wa afua za msingi na kubainisha ufanisi utakaowezesha kufikia malengo kabambe yaliyoainishwa katika sera na nyaraka za kimkakati za Nchi.” Amesema Waziri Ummy

Aidha, Waziri Ummy amesema kupaumbele katika masuala ya VVU/UKIMWI ni pamoja na kulinda mafanikio yaliyofanyika, kupunguza maambukizi mapya hususani kwa vijana balehe pamoja na kupunguza maambukizi mapya kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Amesema, Tanzania imepiga hatua kubwa katika nyanja mbalimbali za mwitikio wa VVU ambapo kwa mujibu wa ripoti ya UNAIDS 2022, Tanzania imefikia Mkakati wa Kimataifa wa UKIMWI 2021 hadi 2026 kwa lengo la matibabu.

“Mafanikio haya yamechangiwa na matokeo ya Utafiti wa Athari za VVU Tanzania Mwaka 2022-2023 (HII 2022-2023) ambao uliripoti kufikiwa kwa malengo ya UNAIDS 95-95-95 kwa 82.7%, 97.9% na 94.3% (ngazi ya jamii).” Amesema Waziri Ummy

“Ikijumuisha 95% ya watu wanaokadiriwa kuwa na maambukizi ya VVU na wanafahamu hali zao za VVU, 95% ya walioambukizwa VVU na wanatumia dawa za kufunaza VVU (ARVs) na 95% ya wale wanaotumia ARVs walifikia hali ya kufunaza VVU.” Amefafanua Waziri Ummy

Mwisho, Waziri Ummy amewashukuru washirika wa Kimataifa wakiwemo PEPFAR, Global Fund, UNAIDS, WHO, UNICEF, CDC, USAID, DOD pamoja na Peace Corps kwa msaada usioyumba wa kiufundi na kifedha katika azma ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kumaliza janga la VVU na UKIMWI ifikapo mwaka 2030.



# Watumishi sekta ya afya wasisitizwa mahusiano mazuri kazini ili kutoa huduma bora kwa wananchi

**Na. Aisha Swahibu**
**RUKWA**

Naibu katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. Grace Magembe amewasisitiza watumishi katika Sekta ya Afya nchini kudumisha Mawasiliano baina yao na wagonjwa ili kujenga mahusiano mazuri baina ya mtumishi na Mgonjwa au ndugu wa mgonjwa.

Ameyasema hayo tarehe 8 Februari, 2024 wakati wa ziara yake ya kikazi Mkoani Rukwa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga iliyolenga kukakua usimamizi wa utendaji kazi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya .

Dkt. Magembe amesema wagonjwa ni vyema kumfanya ajisikie yuko sehemu salama kwa kumpa maelezo juu ya mazingira ya Hospital ni wajibu wa mtoa huduma kumpatia mwelekeo ya kufahamu Mazingira hayo.

“Mgonjwa anapofika hospital au kituo cha afya chakufanya kwa mtoa huduma ni kujitambulisha na muelekeza wa vyumba vya madaktari vilipo, wodi na vyoo hii itamfanya mgonjwa kuwa huru na kutengeneza mahusiano mazuri baina yako na mgonjwa na utamfanya ajisikie yuko sehemu salama, na ndio maana halisi ya huduma bora kwa mteja”

Dkt. Magembe Ameongeza kuwa ni lazima katika kila hospital na vituo vya kutolea huduma za Afya nchini kupandika namba za mawasiliano ili mwananchi anapopata changamoto iwe Rahisi kupata msaada.

“Maelekezo yalishatolewa na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu, Makatibu Wakuu na hata Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tamisemi kuwa katika kila eneo la huduma lazima tubandike namba zetu za simu ili Kama mgonjwa au ndugu wanahitaji maelekezo, kutoa pongezi au kakutana na changamoto ni Rahisi kutoa taarifa yake na kupata msaada “ Amesema Dkt. Magembe

Aidha Dkt. Magembe amesisitia kuwa Mtoa huduma kumpatia taarifa mgonjwa juu ya ugonjwa unaomsumbua na sio kumuacha aondoke bila kujua kinachomsumbua.

“Nisisitize kwenye suala la huduma kwa mteja, unapomfanyia uchunguzi mgonjwa na ukagundua tatizo lake basi mwambie ugonjwa unaomsumbua na hata dawa ulizompa mwambie zitamsaidia kitu gani” amesema.

# MOI yapokea msaada wa mtambo wa upasuaji wenye thamani ya tsh milioni 500.

**Na. Abdallah Nassoro**
**DAR ES SALAAM**

Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Ubongo Muhimbili (MOI) imepokea msaada wa mtambo wa upasuaji wa ubongo kwa njia ya Matundu (ETV Tower) kwaajili ya upasuaji kwa watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi wenye thamani ya Tsh 500 Millioni kutoka Taasisi ya Cure International.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI Prof Abel Makubi amesema vifaa hivyo vitasaidia watoto wengi zaidi kupata huduma ya upasuaji ambapo watoto wawili wataweza kufanyiwa upasuaji kwa wakati mmoja.

Amesema tangu kuanzishwa kwa huduma hiyo MOI miaka 13 iliyopita idadi ya watoto wanaofikishwa hospitalini hapo kwa matibabu imekuwa ikiongezeka na kwamba jitihada zaidi zinahitajika kuhamashisha wananchi kuwapeleka hospitalini watoto hao.

“Hapa nchini, inakadiriwa kuwa watoto 7,500 huzaliwa na matatizo ya vichwa vikubwa na mgongo wazi kila mwaka, kati ya hapo 1,500 tu ndiyo wanaoletwa hospitali kwa matibabu...hapa MOI tangu kuanza kutolewa kwa huduma hizo watoto 7,500 wamefanyiwa upasuaji, haya ni mafanikio makubwa ingawa juhudi zinahitaji kuwafikia watoto wengi zaidi”

Aidha ameishukuru Taasisi ya CURE kwa msaada kwa mtambo huo wa upasuaji na kuahidi kuendeleza ushirikiano baina ya taasisi hizo ili kuendelea kuokoa maisha ya watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi nchini.

Kwa upande wake Meneja Mipango wa CARE Neuro, Joshua Menya amesema msaada huo umelenga kuongeza juhudi za MOI za kutoa huduma kwa watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi.

“Miaka 13 iliyopita tulitoa mashine kama hii, na tumekuja kutoa mashine nyingine, kikubwa tumefurahishwa na huduma za MOI kusaidia watoto hawa ambao jamii wanawaona kama laana. Katika ushirikiano wetu huu pia tulijikita katika kuwajengea uwezo madaktari na sasa ni muendelezo wa vifaa tiba” amesema Menya

Blandina Chande ni muhudumu wa watoto wenye vichwa vikubwa MOI, ametoa wito kwa vijana kuacha tabia ya kutelekeza watoto walemavu na kuwachia mzigo wa kulea wanawake ambao hawana uwezo wa kifedha.

“Watoto hawa wanalelewa na mama, baba ametoroka. Hasa hawa baba vijana ni tatizo sana, niwakumbushe kuwa watoto ni zawadi tuwalee pamoja” amesema Chande



# BMH yapokea magari ya kubebea wagonjwa

**Na. Shaban Juma**
**DODOMA**

Serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imeendelea kuboresha sekta ya afya kwa kutoa magari mawili ya kubebea wagonjwa kwa Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) ya jijini Dodoma ili kusaidia wagonjwa wa kanda ya kati kufika kwa wakati Hospitalini.

Akizungumza baada ya hafla ya kupokea magari hayo, Mbunge wa Dodoma mjini, Mhe. Anthony Mavunde, amesema magari hayo yataondoa changamoto ya wagonjwa wanapopata rufaa.

"Naishukuru Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuboresha sekta ya afya na kuweka mazingira rafiki kwa wananchi kupata Huduma bora za afya",amemshukuru Mhe. Mavunde.

Ameongeza kuwa magari ya kubebea wagonjwa ni muhimu sana kwa BMH kwani Hospitali hii imekuwa kimbilio sio tu kwa wakazi wa Dodoma na kanda ya kati bali kwa watanzania kwa ujumla.

Kwa upande wake Mkuu wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amesema ujio wa magari ya kubebea wagonjwa unaonyesha dhamira ya dhati ya Rais Samia Suluhu Hassan katika kujali afya za watanzania na kutaka taifa lenye afya bora .

"Tutasimamia magari haya yatumike kwa malengo yaliyokusudiwa ambayo ni kubeba wagonjwa ," amesisitiza Mhe. Senyamule

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali, Dkt Alphonce Chandika, ametoa shukrani kwa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuipatia Hospitali hiyo ya Kanda ya Rufaa magari hayo mawili ya kubebea wagonjwa wagonjwa.





# Tanzania mfano mapambano ya kupnguza vifo vitokanavyo na uzazi.

**Na. Abdulwaheed Madenge**
**DODOMA**

Shirika la Maende la Kimataifa la Japani JICA limeitaja Tanzania kama mfano wa kuigwa kwa nchi za Afrika na Duniani kwa ujumla katika mapambano ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kwa kuwa inafanya vizuri kulinganisha na nchi nyingine.

Hayo yamebainika wakati wa uwasilishaji wa mradi kutoka Shirika la ushirikiano wa kimataifa la Japan (JICA) wenye lengo la kufanya uboreshaji wa huduma za mama na mtoto mchanga uliokuwa ukiwasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dkt. John Jingu Februari 14, 2024, Jijini Dodoma.

Mara baada kupoke wasilisho hilo Dkt. Jingu amesema uwepo wa matokeo chanya katika utekelezaji wa mipango na mikakati mbalimbali nchini ndio umekuwa ukihamasisha zaidi wadau kuzidi kuwezesha Miradi zaidi ya kuboresha huduma za afya nchini hasa masuala ya mama na mtoto.

"Tunalishukuru Shirika la Maende la Kimataifa la Japani JICA na Nchi ya Japan kwa misaada inayotoa kwa Tanzania. utekelezaji wa miradi hii utasaidia kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini. Na sisi tunaahidi kutoa ushirikiano utakaohitajika katika utekelezaji wa miradi hii." Amesema Dkt. Jingu

Kwa upande wake Mshauri Mkuu, Idara ya Utafiti na Mipango Bw. Kiyomasa Machida amesema Mradi huo unalenga kuboresha huduma za afya ya mama na mtoto kwa kuimarisha mifumo ya uchunguzi na matibabu ya kikanda kwa kutoa vifaa tiba vinavyohusiana na afya ya mama na mtoto kwa Hospitali za rufaa za mikoa saba (7) Tanzania Bara na Zanzibar/Unguja.

"Hospitali zinazotazamiwa ni Dodoma RRH, Katavi RRH, Ligula RRH, Mount Meru RRH, Sekou Toure RRH, Tumbi RRH, Lumumba RH katika ya Sehemu Ununuzi wa Vifaa vya Matibabu Vifaa vinaweza kutumika kwa huduma za matibabu, utambuzi, matibabu, haswa utunzaji wa mama na mtoto mchanga." amesema Machida

# Waganga wafawidhi mkasimamie huduma bora kwa wananchi - Waziri Ummy

**Na. Majid Abdulkarim**
**DODOMA**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amewataka waganga wafawidhi kusimamia ubora wa huduma za Afya zinazotolewa katika vituo vya Afya nchini ikiwa ni pamoja na kuanzisha madawati ya huduma kwa wateja (Customer Care Desk).

Waziri Ummy amesema hayo Februari 14, 2024 wakati akifunga mkutano wa siku Mbili wa waganga wafawidhi ngazi ya msingi uliofanyika katika mji wa Serikali Mtumba Mkoani Dodoma.

"Kwanza mkasimamie ubora wa huduma ambao ni pamoja na kuanzisha madawati ya huduma kwa wateja (customer care desk) ambazo tunaweza kuanza katika hospitali za Wilaya kwa ajili ya kutatua changamoto za wateja, pili tuimarishe maadili ya watumishi kwa kutoa elimu za mara kwa mara na kuhakikisha kamati za maadili vituoni zinafanya kazi." Amesema Waziri Ummy

Amesema, jambo lingine la kuzingatia kwa waganga hao ni kuhakikisha watumishi walio chini yao wanatoa kauli nzuri kwa wateja kwa kutoa mafunzo ya huduma staha ili wateja waweze kufurahiya huduma kwa kuwa ndio lengo la Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuona Watanzania wanapata huduma bora.

Aidha, Waziri Ummy amemuelekeza Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel kukaa pamoja na Baraza la Madaktari Tanganyika (MCT) kwa lengo la kuangalia matumizi na makusanyo ya fedha za uchangiaji za Chama cha madaktari.

"Tumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan alituelekeza tupunguze fedha za uchangiaji na angalau zimepungua kidgo ambapo kwa mwaka mnalipa Laki Moja na nusu badala ya laki Mbili." Amesema Waziri Ummy.






# Serikali yabainisha vipaumbele 6 vya kisera katika sekta ya afya 2024/25

**Na. Hassan Kimweri**
**DODOMA**

Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maende imebainisha vipaumbele Sita vya kisera katika Sekta ya Afya ambavyo vitawekewa mkazo zaidi katika kutekelezwa kwa mwaka 2024/25 ili kuendelea kuboresha huduma za Afya nchini.

Waziri wa afya Mhe. Ummy Mwalimu amebainisha hayo  Februari 15, 2024 kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kisera wa 23 wa Sekta ya Afya uliofanyika Jijini Dodoma ambapo amesisitiza kipaumbele cha kwanza kuwa ni rasilimali watu katika Afya.

"Serikali imejitolea kuwekeza katika mafunzo na maende ya watumishi wa Afya ili kuhakikisha huduma bora zinapatikana kwa wananchi." Amesema Waziri Ummy

Waziri Ummy amebainisha vipaumbele hivyo ambavyo ni pamoja na Rasilimali watu katika Afya, swala la ubora wa huduma za Afya, utekelezaji wa sheria ya Bima ya Afya kwa wote, wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii, mapambano dhidi ya Magonjwa Yasiyoambukiza na Kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali na Sekta binafsi katika utoaji huduma za Afya.

"Suala la ubora wa huduma za Afya tunaendelea kulisisitiza kwa kuzingatia umuhimu wa kuboresha huduma kwa wateja pamoja na kuhakikisha usalama wao ili mteja apate huduma iliyokua nzuri." Amesema Waziri Ummy

Aidha, katika vipaumbele hivyo Waziri Ummy ametaja utekelezaji wa sheria ya bima ya Afya kwa wote kuwa ni moja ya vipaumbele vya Serikali katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wote ambapo sheria ya Bima ya Afya kwa wote imeshasainiwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan Sasa ni utekeleaji wake.

Waziri Ummy ameelezea juhudi za Serikali katika kuhudumia jamii na kuimarisha huduma za afya ngazi ya jamii, umuhimu wa ushirikiano kati ya Serikali na wadau wengine huku akiongeza kwakusema kuwa Serikali inaongeza nguvu katika mapambano dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza kwa kutoa elimu kwa umma na kuboresha huduma za tiba.

Pia, Waziri Ummy amehimiza umuhimu wa kuzungumzia masuala ya afya ya akili na ajali, na kusisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya Serikali na sekta nyingine katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wote.



# Badilisheni mtindo wa maisha - Prof. Janabi

**Na. Cletus Sanga**
**DAR ES SALAAM**

Serikali kwa kushirikiana na wadau wa Wananchi wameaswa kubadilisha mtindo wa maisha ili kuwa na afya njema na kuepukana na magonjwa yasiyoambukiza.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili Prof. Mohamed Janabi katika hafla ya ugawaji tuzo za HUMANITARIAN AWARD ambazo zimelenga kutambua mchango wa ubinadamu unaofanywa na wadau mbalimbali zilizoandaliwa na shirika lisilo la kiserikali la Professor Jay Foundation Jijini Dar es salaam katika Ukumbi wa Ummy Mwalimu uliopo Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Prof. Janabi amewataka wananchi kubadili mtindo wa maisha ili kuepukana na magonjwa yasiyoambukiza kama Kisukari, Shinikizo la Damu, Kiharusi, Ugonjwa wa Figo.

"Kinga ni Bora kuliko tiba ni vyema kupunguza matumizi ya sukari pia haina haja ya kwenda 'gym' unaweza kutembea angalau hatua 10 kwa siku, hakuna chakula tunasema usile, kula kwa kiasi ila kula vyakula vyenye Afya, punguza kula vyakula vya kusindika". Amesema Prof. Janabi

Nae mwakilishi kutoka Wizara ya Afya Bi. Grace Msemwa amesema Wizara ina jukumu la kuelimisha na kuhamasisha jamii juu ya masuala mbalimbali ya afya ikiwemo mabadiliko chanya ya tabia na kufanya uchunguzi wa awali wa afya.

"Jamii iendelee kufuatilia taarifa sahihi za namna ya kujikinga na Magonjwa yasiyoambukiza na yanayoambukiza, ili kupata taarifa hizo kwa usahihi wananchi wanashauriwa kupiga simu namba 199 bure. Amesema. Bi Grace.

Aidha, Bi Grace amepokea tuzo iliyotolewa kwa Wizara ya Afya kutokana na mchango mkubwa katika utoaji wa Elimu kwa jamii kuhusu Afya.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo @Professorjayfoundation Bw. Florian Rutabingwa ameelezea ujio wa program maalumu inayoandaliwa kwa ushirikiano mkubwa na wizara ya afya kupitia Sehemu ya Elimu ya Afya kwa umma, 'AFYA NA MUZIKI TOUR' ambayo inalenga kuzunguka nchi nzima kutoa elimu ya afya kwa wananchi kuhusu magonjwa yakuambukizwa na yasiyoambukizwa lakini pia kuwezesha upimaji wa afya kwa wananchi hususani kwenye magonjwa yasiyo ya kuambukizwa.




# Serikali inatambua mchango wa sekta binafsi katika kuwahudumia wananchi

**Na. Hassan Kimweri**
**DAR ES SALAAM**

Serikali kupitia Wizara ya Afya imebainisha kuwa inatambua na kuthamini mchango wa Sekta binafsi katika nyanja zote kupitia utekelezaji sera ya ubia kati ya Sekta za Umma na Binafsi (P-P-P) ambapo imevutiwa na uwekezaji unaofanywa nchini.

Hayo yamesemwa na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu  Februari 18, 2024 kwenye uzinduzi wa Hospitali ya Saifee iliyozinduliwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa jijini Dar Es Salaam.

“Sisi Kama Serikali tunashirikiana na Hospitali zote binafsi ikiwemo hii ya Saifee katika kuvutia wagonjwa kutoka nje ya nchi na tunaendelea kuondoa vikwazo vinavyokwaza Sekta binafsi katika kutoa huduma za Afya nchini.” Amesema Waziri Ummy.

Waziri Ummy Mwalimu amesema, Serikali inaendelea kushirikiana na Sekta Binafsi ikiwemo Hospitali hiyo ya Saifee katika kuvutia wagonjwa kutoka nje ya nchi ambapo hivi sasa zipo Hospitali Sita zinazotoa huduma za Tiba Utalii ikiwemo za Serikali na binafsi.

“HospitalI hizo ni pamoja na Muhimbili, MOI, JKCI, Ocean Road, Saifee na Aga Khan ambapo Hospitali hizo zimeweza kuona na kutibu wagonjwa kutoka nje ya nchi kwa mwaka 2022 walionwa wagonjwa 5,705 na mwaka 2023 wameongezeka na kufikia wagonjwa 6,931 waliopata matibabu sawa na ongezeko la wagonjwa 1,226.” Amesema Waziri Ummy

Mwisho, Waziri Ummy ametoa rai kwa Watanzania kuzingatia mtindo bora wa maisha ikiwemo kufanya mazoezi, kuacha matumizi ya vyakula kwa kuongeza mafuta mengi, chumvi nyingi na sukari kupita kiasi.

“Hata kama tutajenga hospitali 100 kama hizi za Saifee tusipobadili mtindo wetu wa maisha hospitali hazitatosha tusifanye mzaha na ushauri tunaopata kutoka kwa wataalamu wa Afya akiwemo Dkt. Janabi.” Amesema Waziri Ummy

# Toeni huduma bora za afya kuipa thamani miradi na uwekezaji wa serikali katika sekta ya afya

**Na. Shaban Juma**
**MWANZA**

Serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan Watumishi na watoa huduma za afya wamesisitizwa kuzingatia weledi na miiko ya taaluma zao wanapotekeleza majukumu yao ili kuipa thamani Miradi na uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali katika sekta ya Afya Nchini.

Msisitizo umetolewa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. Grace Magembe Februari 20, 2024 wakati wa ukaguzi wa Miradi ya ujenzi na usimikaji vifaa tiba inayoendelea katika Hospitali ya Rufaa Mkoa Sekou Toure, Hospitali ya Halmashauri ya Jiji la Nyamagana na Hospitali ya Kanda Bugando zote za Mkoani Mwanza. Amesema Serikali inatoa fedha nyingi katika kuboresha hali ya utoaji wa huduma za Afya nchini lakini kumekuwapo na baadhi ya watoa huduma ambao sio waadilifu na kufanya jitihada hizo zisionekane.

"Ndugu zangu huu uwekezaji ni mkubwa sana kutokea katika miaka 3 iliyopita. Mhe. Rais Dkt Samia Suluhu Hassan amefanya jukumu lake, kazi iliyobakia ni sisi kutekeleza wajibu wetu na hasa watoa huduma za Afya, tubadilike tuache kufanya kazi kwa mazoea, kila taaluma katika sekta ya afya inayo miiko yake lazima kila mtu afanye kazi kwa kuzingatia miiko na weledi wa taaluma yake" amesema Dkt. Magembe.

"Hakutakuwa na kupepesa macho, tutachukuliana hatua, tutatoa nafasi ya kufundishana, kuelekezana na kurekebishana, yote hayo yakishindikana tutachukua hatua kali zaidi. Tumeshuhudia baadhi ya wenzetu ambao wamefutiwa usajili na mabaraza yao ya taaluma, wamesimamishwa kazi kwa miaka kadhaa, wengine wamerudishwa vyuoni" na wengine kufukuzwa kazi kabisa amesema Dkt. Magembe.

Aidha Dkt. Magembe amesema Serikali itawapa motisha mbalimbali watoa huduma ambao watafanya vizuri ikiwa ni sehemu ya kutambua utendaji wao mzuri wa kazi.

Naibu Katibu Mkuu yuko ziarani kanda ya Ziwa kukagua utekelezaji wa miradi ya Afya na utoaji wa huduma.



# Tafiti zote zinazohusu chakula na lishe kufanyiwa uchunguzi wa kimaabara



**Na. Englibert Kayombo**
**DAR ES SALAAM**

Serikali kupitia Wizara ya Afya imepanga kuweka sharti kwa kufanya uchunguzi wa kimaabara kwenye tafiti zozote nchini zinazohusisha masuala ya chakula na lishe katika Maabara ya Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC).

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amesema hayo  Februari 20, 2024 wakati wa ziara yake ya kukagua na kuona kazi zinazofanywa na Taasisi ya Chakula na Lishe kwa upande wa Maabara iliyopo Mikocheni Jijini Dar Es Salaam.

"Tunampango wa kufanya uchunguzi wa kimaabara kwa mtu yeyote au shirika lolote linalofanya tafiti zinazohusu masuala ya chakula na lishe, lazima zithibitishwe na ushahidi wa kisayansi baada ya sampuli kuchukuliwa na kuletwa katika maabara hii, isiwe tu ni tafiti za kwenye makaratasi." Amesema Waziri Ummy.

Waziri Ummy Mwalimu amesema maabara hiyo ya chakula na lishe ni moja ya maabara kubwa na zinazoaminika katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika ambapo amefurahishwa na kazi wanazofanya ikiwa ni pamoja na kuja na ushahidi wa kisayansi.

"Lakini pia kuna utafiti ambao wameufanya na kushauri kwamba wataalamu wa Afya wanashauri na kuelekeza watoto wa umri chini ya miezi Sita wasipewe chakula kingine chochote zaidi ya maziwa na mama". Amesema Waziri Ummy.

Maabara hiyo imegawanyika katika sehem Tatu ambayo ni maabara ya chakula (food chemistry) ambayo inafanya uchunguzi wa viinilishe (macro and micro nutrients), maabara inayofanya uchunguzi wa viashiria vya viini lishe mwilini (micronuient biomarkers), na maabara inayofanya uchunguzi wa hali ya lishe (body composition) ikiwa ni pamoja na kugundua kama chakula kimeharibika.

Mwisho, Waziri Ummy ametoa wito kwa Watanzania kuzingatia mtindo bora wa maisha kwa kufanya mazoezi, kupunguza matumizi ya sukari na chumvi ili kuepuka kupata magonjwa yasiyoambukiza kwa kuwa yamekuwa yakiongezeka kila siku.

# Tuendelee kuboresha ubora wa huduma za afya

**Na. Said Nyaoza**
**DAR ES SALAAM**

zaidi ubora wa huduma za afya zinazotolewa katika Taasisi hiyo ili uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali uwe na tija katika huduma bora zinatolewa MOI.

Hayo yamesemwa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo Dkt. Faustine Ndugulile Februari 22, 2024 akiiongoza Kamati hiyo kufanya ziara ya kuona hali ya utoaji huduma za Afya, maboresho ya miundombinu ya kutolea huduma ikiwemo na miradi ya afya inayotekelezwa na Taasisi hiyo.

"Tunawapongeza MOI, hongereni sana mko katika mwelekezo sahihi, Kamati imeridhika na hali ya utoaji huduma tunawapongeza sana, endeleeni kuboresha zaidi ubora wa huduma mnazozitoa hapa"amesema Dkt. Ndugulile.

Wajumbe wa kamati hiyo walipata fursa ya kutembelea kitengo cha radiolojia kinachojihusha na vipimo vya CT -Scan, MRI na X-Ray, pia walitembelea kitengo cha huduma za wagonjwa maalum na wa kimataifa, jengo la kusubiria wagonjwa na wodini, ambapo walipata nafasi ya kuwapa pole wagonjwa na kusikiliza maoni yao.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel amesisitiza Uongozi wa Taasisi ya Mifupa MOI kuweka usimamizi mzuri wa utoaji huduma kwa kuwasimamia vyema watumishi ngazi za chini yao.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa MOI Prof. Abel Mkabi amesema uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali ya awamu ya Sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambao umewezesha kuboresha hali ya utoaji wa huduma katika Taasisi ya MOI.

"Kutokana na uwekezaji uliofanywa na serikali ya awamu ya sita, tumeweza kuongeza idadi ya oparesheni kufikia 30 hadi 40 kwa siku huko nyuma tulikuwa tunafanya operesheni 20, tunamshukuru Mh. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan" amesema Prof. Makubi na kuongeza

"Tumeweza kupunguza rufaa za wagonjwa kwenda kutibiwa nje ya nchi kwa asilima 97 kwa wagonjwa wa ubongo na asilimia 99 kwa wagonjwa wa mifupa" amesema Prof. Makubi.





# Kuwait imekua msaada kwa tanzania katika Sekta ya Afya

**Na. Hassan Kimweri**
**DAR ES SALAAM**

Serikali ya Kuwait imekuwa msaada kwa Serikali ya Tanzania katika Sekta ya Afya ambapo imeweza kusaidia mipango kadhaa ikiwa ni pamoja na kutoa msaada wa mashine za ganzi kwa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Uwalimu amesema hayo  Februari 21, 2024 Jijini Dar Es Salaam kwenye Maadhimisho ya Miaka 63 ya Uhuru na miaka 33 ya Siku ya Ukombozi wa Kuwait ambapo kwa Tanzania Maadhimisho hayo yameongozwa na Balozi wa Kuwait nchini Mhe. Mubarak Mohammad Alsehaijan.

“Kwa nafasi yangu kama Waziri wa Afya, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuishukuru Serikali ya Kuwait kwa msaada wake katika Sekta ya Afya, pamoja na kutoa msaada wa mashine za ganzi, wameweza kusaidia vifaa vya upasuaji kwa watoto wanaosumbuliwa na vichwa vikubwa (Hydrocephalus) kwenda Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI).” Amesema Waziri Ummy

Amesema, Kuwait imesaidia pia kwa kutoa Vifaa Tiba katika Hospitali ya Mnazi Mmoja Zanzibar, Mashine za Watoto Wachanga zisizo na hewa kwa Hospitali ya Benjamin Mkapa mjini Dodoma pamoja na ujenzi wa Hospitali ya Handeni, Tanga unaofadhiliwa na Taasisi ya Abdullah Al Nouri ya Kuwait.

Aidha, kwa mwaka 2023 Kuwait kupitia Kuwait Children Heart Association ilileta madaktari bingwa walioshirikiana na wataalam wa Hospitali ya Benjamin Mkapa Dodoma na kufanya upasuaji wa moyo bure kwa watoto 100 wa kipato cha chini nchini.

“Hatua hizi zinaashiria kwamba uhusiano wa kindugu na urafiki uliopo kati ya nchi zetu mbili (Tanzania na Kuwait), nina imani kuwa uhusiano huu utaendelea kuwa wa karibu na chini ya uongozi wa busara, mahiri na mwanga wa viongozi wetu wawili, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Sheikh Mishal al-Ahmad al. -Sabah, Amir wa Kuwait.” Amesema Waziri Ummy

# Mafanikio ya Tanzania kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi yaivutia nigeria

**Na. Aisha Swahibu**
**DODOMA**

Mafanikio katika sekta ya Afya katika kukabiliana na kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, mama na mtoto kumepelekea baadhi ya mataifa mengine ya Afrika kuja kujifunza nchini.

Hayo yamesemwa na Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. John Jingu tarehe 22 Februari, 2024 Jijini Dodoma wakati wa kikao na wajumbe kutoka Serikali ya Nigeria uliongozwa na Kamishina wa Afya wa jimbo la Borno Prof. Baba Gana, waliokuja kwa lengo la kujifunza njia za kupunguza vifo vya uzazi na mtoto kupitia mfumo wa M-mama.

Dkt. Jingu amesema mafanikio haya ambayo Serikali imeyapata ni kutokana na jitihada na bunifu mbalimbali katika kukabiliana na vifo vya mama na mtoto, na matokeo yameonekana na kufanya Tanzania kuwa sehemu iliyovutia mataifa mengine kuja kujifunza.

“Takwimu zinaonyesha mwaka 2015 vifo vya watoto wachanga vilikuwa ni 556 kati ya vizazi hai laki 100,000 namba hizi zimeshuka kufikia vifo 104 kwa vizazi hali laki 100,000 kwa mwaka 2023 kwa hiyo wenzetu wakajiuliza tumefanyaje, tumewaambia hii ni kutokana na uongozi imara wa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassani ambae amekuwa ni kinara katika kuhakikisha afya za mama na mtoto zinalindwa kwa kuwa na miundombinu wezeshi na kufanya kazi kwa ubora kote nchini na kuwa na watumishi wanaofanya kazi kwa weledi. Amesema Dkt. Jingu.

Amesema Serikali imeweka mkakati wa kuzuia vifo vinavyotokana na uzazi mama na mtoto mchanga na kwamba havikubaliki kwa sababu njia za kuvizuia zipo na zinatekelezeka kwa kuwa na jitihada na ubunifu wa uzazi salama ambao unashirikisha jamii.

“Tanzania tuna mfumo mpya wa uzazi salama ambao kwa sasa uko katika Halmashauri 30 kwenye hatua za majaribio na baadae tutaendelea na awamu ya pili katika Halmashauri 110, lengo likiwa ni kuhakikisha wadau muhimu ambao ni jamii wanashirikishwa kikamilifu”. Amesema Dkt. Jingu.

Kwa upande wake Kamishna wa Afya jimbo la Borno Prof. Baba Gana amesema nchi ya Nigeria bado haijapiga hatua kwenye kuzuia vifo vinavyotokana na uzazi hivyo wamevutiwa na jitihada za Serikali ya Tanzania na kuja kujifunza.






# Rais Samia anaendelea kutoa fedha kutatua kero katika sekta ya elimu, afya na miundombinu

**Na. Abdulwaheed Madenge**
**TANGA**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea kutoa fedha nyingi katika kutatua kero za Watanzania ikiwemo wananchi wa Mkoa wa Tanga na katika Sekta ya Maji ambapo ametoa Billioni 25 kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa maji safi na salama katika Jiji la Tanga na maeneo ya pembezoni.

Hayo yamesemwa Februari 22, 2024 na Waziri wa Afya na Mbunge wa Jimbo la Tanga Mjini Mhe. Ummy Mwalimu kwenye ziara ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Isdor Mpango wakati akizindua hati fungani ya kijani ya miundombinu ya maji Mkoani Tanga.

Waziri Ummy Mwalimu amemshukuru Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan Kwa kutoa fedha nyingi kwa ajili ya kutatua kero za wananchi wa Mkoa wa Tanga katika Sekta ya Elimu, afya, barabara na maboresho ya Bandari ya Tanga.

Aidha, Waziri Ummy amesema, Kwa upande wa Sekta ya Afya, Jiji la Tanga lina vituo Sita vya Afya ambavyo vinafanya kazi.

"Kwa upande wa Hospitali za Rufaa tumesambaza mashine za kisasa za uchunguzi ikiwemo CT-Scan katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara ikiwa ni pamoja na hospitali ya Rufaa ya Bombo Tanga". Amesema Waziri Ummy.

Amesema, wananchi wa Mkoa wa Tanga sasa hivi hawana haja ya kwenda tena Dar Es Salaam au Kilimanjaro kwa ajili ya kufata huduma za CT-Scan au huduma za kusafisha damu, huduma zote hizo zinapatikana Mkoani hapo.

"Hatua hii ni kubwa ambayo Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya ya kuwajali wananchi wake katika maendelea na sasa kwenye sekta ya maji Rais Samia atatupatia Bilioni 53 kwa ajili ya mradi wa upatikanaji wa maji kwa asilimia 100 kwa wakazi wa Tanga Mjini pamoja na Wilaya jirani za Muheza na Mkinga". Amesema Waziri Ummy.

Katika hatua nyingine, Waziri Ummy ametoa rai kwa Watanzania kuzingatia mtindo bora wa maisha kwa kufanya mazoezi angalau dakika 40 kwa siku mara nne kwa wiki, kupunguza matumizi ya Sukari, Chumvi na Mafuta.

Mradi huo wa maji uliozinduliwa utazalisha wastani wa jumla ya lita Milioni 60 kutoka lita 45 za awali katika Mkoa wa Tanga.

# Tutengeneze wasomi wenye akili vumbuzi siyo akili kibarua-dkt. Mollel

**Na. Majid Abdulkarim**
**DODOMA**

Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel amewataka wasomi nchini kubadili fikra zao kwa kutumia akili vumbuzi na sio akili kibarua ili kulisaidia taifa kusonga mbele kwa maende.

Dkt. Mollel amesema hayo  Jijini Dodoma wakati akijibu swali Namba 223 kwa niaba ya Waziri wa Afya, Mhe. Ummy Mwalimu lililoulizwa na Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi Mhe. Ameir Abdallah Ameir aliyeuliza Je, ni tafiti zipi ambazo Taasisi za Tiba Asili zimekamilisha na kuweza kuwa suluhisho la maradhi mbalimbali kama Tiba Mbadala.

Dkt. Mollel amesema kuwa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 – 2024 zaidi ya tafiti 50 zimefanyika ndani ya nchi juu ya ubora na usalama wa dawa zinazotumika kwa tiba asilia kwa kupitia Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR).

Ameongeza kuwa baadhi ya tafiti hizo ni pamoja na utafiti wa dawa ya Saratani ya NIMREGENIN, Dawa ya TANGHESHA inayotibu Selimundu, Dawa ya PERVIVIN inayotibu tezi dume, Dawa ya WARBUGISTAT inayotibu magonjwa nyemelezi na Dawa ya NIMRICAF inayotibu Mfumo wa upumuaji.

Aidha, Dkt. Mollel ametoa wito kwa wananchi kuhakikisha wanatunza miti inayotumika kutengeneza dawa za tiba asili ili kuendelea kuzalisha dawa za tiba asili za kutosha nchini. Amesema Waziri Ummy






# Wasajili wa mabaraza ya taaluma na bodi watakiwa kuongeza ufanisi kusimamia sekta ya afya

**Na. Abdulwaheed Madenge**
**DODOMA**

Wasajili wa Mabaraza ya Wataalamu na Bodi za Ushauri nchini wametakiwa kuweka mikakati na mifumo yenye tija itakayohakikisha wanataaluma wanazingatia weledi na Miiko ya taaluma zao ili kuongeza ubunifu katika utendaji na kuhakikisha watanzania wanapata hubuma bora za Afya nchini.

Hayo yamesemwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dkt. John Jingu Februari 22, 2024 jijini Dodoma katika kikao na Wasajili wa Mabaraza ya wataalam na Bodi ya Washauri kilichokua na lengo la kujadili namna ya kuzidi kuboresha huduma kwa wananchi.

Dkt. Jingu amewataka wasajili hao kuweka mifumo mahali pa kutolea huduma itakayowezesha kuibua upotovu wa Maadili au ukosefu wa weledi kwa wanataaluma kwa wakati hasa kwa kuwashirikisha viongozi wa ngazi za Mikoa.

Aidha, Dkt. Jingu amewataka wasajili hao kubaini na kuzizuia Changamoto za Maadili na weledi kabla hazijaleta madhara makubwa na wasibaki kuwa kama mahakimu wa kusubiri hadi matatizo yatokee ndio wachukue hatua.

"Gatueni majukumu yenu huko katika Mikoa na Halmashauri kwa kuzingatia sheria zilizounda Mabaraza yenu lakini kufanya hivyo hakuwaondolei majukumu yenu, bado mna jukumu la msingi la kusimamia weledi na Maadili ya wanataaluma katika Sekta yetu ya Afya". Amesema Dkt. Jingu.

Ameongeza kuwa Wananchi wanastahili kupata huduma bora hivyo wasajili wanapaswa kufuatilia na kufanyia kazi kero za wananchi ikiwa ni pamoja na malalamiko ili.kuongeza tija na ufanisi wa utendaji.

Dkt. Jingu ameelekeza mabaraza kujitangaza ili majukumu yake yajulikane na kuwawekea wananchi namna nzuri ili waweze kufika katika mabaraza kwa urahisi ili kutoa taarifa".

"Twendeni tukawajulishe wananchi kuwa sisi ni akina nani, majukumu yetu ni yapi na njia na mawasiliano zinazotumika ili kutufikia". Amesema.

Dkt. Jingu amewataka wasajili hao kuacha kufanya kazi kwa nyezo za kizamani bali wazingatie na kutekeleza majukumu kwa kutumia teknolojia za kisasa za mawasiliano ili kuongeza uwajibikaji.

# Huduma za Dharura zaokoa maisha ya wananchi mkoani Simiyu

**Na. Shaban Juma**
**SIMIYU**

Serikali ya awamu ya sita chini ya Uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kuimarisha sekta ya afya kwa kujenga majengo ya Huduma za dharura 101 katika maeneo mbalimbali nchini ambapo Mkoa wa Simiyu ni kati ya Mikoa iliyofaidika.

Hayo yamebainishwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. Grace Magembe Februari 23, 2024, wakati wa ziara yake akiwa Mkoani Simiyu alipotembelea Hospitali ya Wilaya Bariadi na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Simiyu kujionea mafanikio ya majengo hayo tangu kuanzishwa kwake ambapo wagonjwa pamoja na majeruhi zaidi ya 200 wameshahudumiwa kwenye hospitali hizo mbili.

Katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Simiyu, Dkt. Magembe alijionea namna jengo la dharura linavyoweza kuhudumia majeruhi wengi kwa pamoja (Mass Casualities) na kuwapanga kutokana uhitaji wa haraka wa huduma (Triaging) ili kuokoa maisha kwa haraka.

“Jengo la huduma ya dharura limekuwa na umuhimu mkubwa tangu kuanza kutoa huduma mwezi Agosti 2023. Mpaka kufikia Februari 2024, jumla ya wagonjwa 191 wa dharura wamepatiwa huduma katika jengo hili. Hii imepunguza mzigo kwa wagonjwa ambao hapo awali walilazimika kusafiri umbali mrefu kwenda kupata huduma hiyo”. Amesema Dkt. Magembe.

Kwa upande wake Mkuu wa huduma za dharura Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu Dkt. Juma Munna amesema Hospitali hiyo inapokea dharura zote kati ya 40 hadi 50 kwa siku wakiwemo watoto na watu wazima.

"Utaona kuna dharura za ajali, upasuaji, walioumia kichwani, dharura za magonjwa ya ndani na mlipuko. Tunawachukua taarifa zote za muhimu na vipimo vya dharura wakiwa hapahapa, hadi wakihitaji X-ray tunayo mashine inayotembea (Mobile X-ray) kwa wale walioumia sana na hawawezi kusafirishwa kirahisi kwenda jengo la mionzi". amesema Dkt. Juma Munna.

Nae Mganga mfawidhi wa Hospitali ya Halmashauri ya Bariadi Dkt. Flavian Jacob Rweyungura amesema Haya ni mapinduzi makubwa katika kuokoa maisha ya wananchi kwa kuwapunguzia wananchi umbali wa kupata huduma.





# Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI yamepungua kufikia asilimia 1.7 mkoa wa lindi

**Na. Hassan Kimweri**
**LINDI**

Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI yamepungua katika Manispaa ya Mkoa wa Lindi kutoka asilimia 2 hadi asilimia 1.7 Mwaka 2023 ambayo imepelekea kufikia malengo ya 95-95-95 katika Mkoa huo huku viongozi wa Mkoa huo wametakiwa kutobweteka waendelee kuchukua hatua kwa kutoa elimu.

Wazir Ummy Mwalimu amesema hayo jFebruari 29, 2024 akiwa katika ziara yake ya kikazi katika Mkoa wa Lindi baada ya kutembelea katika kituo cha Afya Mnazi mmoja, kituo cha Afya cha Mjini, Zahanati ya Nachingwea pamoja na kutembelea Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi.

"Niwapongeze Mkoa wa Lindi Mmefikia malengo ya 95-95-95 ambapo asilimia 96 ya watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI wanajua kwamba wana maambukizi ya UKIMWI, asilimia 95 ya watu wenye maambukizi wapo kwenye dawa na katika asilimia hiyo 95 ya wanaotumia dawa Virusi vimefubazwa." Amesema Waziri Ummy

Aidha, Waziri Ummy amewataka wananchi kuzingatia mtindo bora wa maisha ikiwemo kufanya mazoezi, ulaji wa vyakula kwa kupungua chumvi nyingi, sukari nyingi na mafuta mengi ili kuepuka kupata magonjwa Yasiyoambukiza ikiwemo Kisukari.

"Miaka Mitano iliyopita huwezi kuona Kisukari, huwezi kuona shinikizo la juu la damu kwenye magonjwa matano yanayowasumbua Watanzania wengi." Amesema Waziri Ummy

Waziri Ummy anatarajia kumaliza ziara yake ya kikazi Mkoani Lindi  Machi 1, 2024 baada ya kutembelea katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi (Sokoine) pamoja na kuzungumza na Kamati ya Afya Ngazi ya Mkoa (RHMT)na Kamati ya Afya Ngazi ya Wilaya (CHMT)

# Serikali na usaid kushirikiana kutimiza vipaumbele vya sekta ya afya



**Na. Abdulwaheed Madenge**
**DODOMA**

Serikali kupitia Wizara ya afya imeadhimia kuendelea kushirikiana na shirika la Kimataifa la Maendeleo la Marekani USAID kwa mwaka 2024/2025 kusaidiana kutimiza vipaumbele vya sekta afya na kuboresha hali ya utoaji wa huduma za afya Nchini.

Hayo yamebainishwa Februari 29, 2024 na Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. John Jingu wakati wa kikao cha mapitio ya portfolia kati ya Serikali ya Tanzania na Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID) ambapo amesema katika kuboresha huduma za afya na kuondokana na changamoto ambazo ni kikwazo kwa wananchi ni muhimu kutambua mchango wa wadau wa afya na maendeleo

Dkt. Jingu amesema USAID imekuwa ikishirikiana na Serikali ya Tanzania katika nyanja mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Uzazi wa Mpango, Afya ya Kina Mama na Watoto, Usalama wa Afya wa Kimataifa, usimamizi wa ugavi, na mifumo ya taarifa za afya.

"Kwa miaka mingi, Serikali ya Tanzania na USAID wamekuwa wakishirikiana katika miradi mbalimbali ya afya, ikiwa ni pamoja na mipango ya kupambana na VVU na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria, Uzazi wa Mpango,

Afya ya Kina Mama na Watoto, kuimarisha mfumo wa afya, na Usalama wa Afya wa Kimataifa. Kwa msaada wa USAID, Serikali ya Tanzania imefanikiwa kupanua huduma kamili za VVU katika mikoa 14". Amesema Dkt. Jingu

Aidha amebainisha ni muhimu kwa USAID kuelewa vipaumbele vya afya vilivyowekwa na Serikali ya Tanzania ili kuongeza athari yetu pamoja na kukuza mabadiliko muhimu katika kushughulikia pengo la Rasilimali Watu kwa Afya, kutekeleza bima ya afya ya kimataifa, kuboresha ubora wa huduma za afya, kusaidia Watoa Huduma za Afya za Kijamii, kupambana na Maradhi Yasiyoambukiza, na kuimarisha ushirikiano wa umma na binafsi.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Misheni ya USAID Bw. Craig Hart amesema Shirika la Maendeleo la USAID litaendelea na ushirikiano katika kuleta matokeo chanya na yenye athari katika afya na ustawi wa Watanzania.

# NHIF yafanya maboresho ya kitita cha mafao kwa wanufaika wake, utekelezaji kuanza machi 01, 2024

**Na. Englibert Kayombo**
**DAR ES SALAAM**

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umefanya maboresho ya Kitita cha Mafao kwa wanachama wake ambayo utekelezaji wake utaanza rasmi Machi 1, 2024.

Hayo yamebainishwa Februari 28, 2024 na Mkurugenzi Mkuu wa NHIF Bw. Bernard Konga akizungumza na waandishi wa habari Dar Es Salaam kwa lengo la kuutaarifu umma juu ya maboresho hayo.

"Kitita cha mafao ni orodha ya huduma za matibabu ambazo zinatolewa kwa wanufaika wa NHIF na bei zake ambazo hutumika wakati wa malipo kwa madai ya watoa huduma za matibabu. Maboresho ya mwisho ya kitita cha mafao cha NHIF kinachotumika sasa yalifanyika Juni, 2016 takriban miaka nane iliyopita na hivyo kuwepo kwa umuhimu wa kufanya marejeo yake kutokana na sababu mbalimbali kama zinavyoanishwa kwenye taarifa hii," amesema Konga.

Konga ametaja malengo ya maboresho ya kitita cha mafao kuwa ni kuboresha upatikanaji wa huduma bora kwa wanachama ikiwa ni pamoja na kuongeza huduma ambazo hazikuwepo awali, Kufanya maboresho ya huduma na gharama zake kwa kuzingatia maende ya teknolojia na hali halisi ya bei katika soko na Kuwianisha Kitita cha Mafao na miongozo ya tiba iliyoboreshwa ili kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa wanufaika wa Mfuko.

Malengo mengine ni Kujumuisha maoni na mapendekezo mbalimbali ya Wadau, Kutekeleza ushauri wa Taarifa ya Mapendekezo ya Tathmini ya Uhai na Uendelevu wa Mfuko kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2021 na Kuimarisha udhibiti katika mianya ya udanganyifu.

Konga ameeleza kuwa Mfuko ulianza zoezi la kufanya marejeo ya kitita kuanzia mwaka 2018, hata tenhivyo utekelezaji wa kitita kipya haukufanyika kutokana na uhitaji wa kuhusisha wadau zaidi ili kuwa na uelewa na maoni zaidi kuboresha kitita hicho.

Maboresho ya Kitita cha Mafao yamehusisha kufanyika kwa Tathmini ya Uhai na Uendelevu wa Mfuko na kutekeleza mapendekezo yake ambapo tathmini ya mwisho ilifanyika Juni, 2021 ambapo Kifungu Na 15.2 cha Mkataba baina ya Mfuko na Watoa Huduma kinautaka Mfuko kutoa notisi ya miezi mitatu (3) ya kusudio la kufanya maboresho katika kitita chake kabla ya kuanza kutumika.





# Watumishi wametakiwa kushirikiana ili kutoa huduma bora kwa wananchi

**Na. Aisha Swahibu**
**DODOMA**

Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. John Jingu amewataka watumishi katika sekta ya Afya nchini kufanya kazi kama timu na kudumisha ushirikiano ili kuzidi kuimarisha na kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma bora kwa Watanzania.

Dkt. Jingu ameyasema hayo tarehe 24, 2024 jijini Dodoma wakati wa ziara yake ya kikazi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Dodoma ili kukagua utendaji kazi na kuzungumza na watumishi wa hospitali hiyo ambapo ameambatana na Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu na Mganga Mkuu wa Mkoa Dkt. Best Magoma.

“Kwenye timu kuna namba tofauti tofauti, hapa tuna madaktari, wauguzi, wahudumu, watu wa utawala kila mmoja ana jukumu lake, tufanye kazi kama timu maana hii Hospitali yetu hata kama ina rasilimali nzuri kiasi gani kama hamfanyi kazi kama timu basi hamtaweza kufanya vizuri. Amesema Dkt. Jingu.

Dkt. Jingu ameelekeza Hospitali, zahanati na vituo vya kutolea huduma za afya nchini kuimarisha huduma kwa mteja na kuunda mfumo wa dawati la kusikiliza maoni, kero na malalamiko kwa wateja na kuwa na watoa huduma wenye weledi wenye kutumia lugha nzuri za staha pamoja na kulinda na kuzingatia haki za wagonjwa ikiwemo kutunza siri za wagonjwa .

Ni jukumu la kila mtumishi kuwahudumia wagonjwa sawa sawa kwa sababu tunategemea kila anaekuja kupata huduma ni mgonjwa hivyo huenda akawa na hasira ila unatakiwa kumuhudumia na kumpokea vizuri na nilitoa maelekezo kwa Hospitali zetu zote kuanzishwa kwa dawati la kusikiliza maoni, kero na malalamiko ya wateja ambalo linaonekana na kufikika na watoa huduma muda wote na wenye weledi na watakao kuwa na lugha za staha zinazozingatia mila na desturi zetu za kitanzania ikiwemo kutunza siri za wagonjwa". Amesema Dkt. Jingu.

Dkt. Jingu amepongeza watumishi wa Hospitali hiyo kwa ubunifu wa utoaji wa huduma bora na nzuri wagonjwa, usafi wa mazingira ya hospitali na ushirikiano walioutoa wakati wa janga la maporomoko ya Wilaya ya Hanang.

”Niwapongeze kwa ubunifu mlioufanya katika kila kitengo kuhakikisha huduma zote zinapatikana na kujitosheleza".



# Kamati ya Bunge yaridhishwa na huduma bora Mloganzila

**Na. Emmanuel Malegi**
**DAR ES SALAAM**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Maswala ya UKIMWI imeridhishwa na hali ya utoaji huduma katika Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila kuanzia kwa wafanyakazi, vifaa bora na vya kisasa vya kutolea huduma ambapo pia mazingira yanaridhisha na wagonjwa wanahudumiwa vizuri.

Hayo yamebainishwa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, Dkt. Faustine Ndugulile baada ya ziara ya kamati ya kutembelea hospitali hiyo na kukagua maboresho ya miundombinu iliyofanywa na Serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Dkt. Ndugulile amesema Serikali imefanya uwekezaji mkubwa wa kujenga hospitali hiyo ambapo pia kuna kituo kingine cha utafiti wa magonjwa ya moyo ambacho kimejengwa katika eneo hilo.

"Niipongeze Serikali kwa kuboresha huduma za afya nchini kwani hivi sasa asilimia 90 ya wagonjwa ambao walikuwa wanakwenda nje ya nchi kutibiwa wanatibiwa hapa nchini na tumeanza kupata wageni kutoka nje ya nchi kuja kupata huduma nchini". Ameeleza Dkt. Ndungulile.

Aidha, ameitaka Serikali kupanua wigo wa utoaji huduma katika hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila kwani hospitali hiyo bado ina eneo kubwa ambapo kuna takribani ekari 3800.

"Tunahitaji upanuzi wa huduma za magonjwa ya moyo, upanuzi wa huduma za saratani, upanuzi wa huduma za magonjwa mengine ya mifupa na mfumo wa ubongo ili wananchi waweze kupata huduma bora na rahisi kwa wepesi zaidi hapa nchini". Amesema Dkt. Ndugulile.

Vile vile ameongeza kuwa kuna fedha wameambiwa zimepatikana, ujenzi unashindwa kuendelea kwa sababu ya masuala ya umiliki wa ardhi hayajakamilika hivyo kamati hiyo imeitaka Serikali kupitia Wizara ya afya na Wizara ya Elimu kukaa pamoja ili kuweza kufikia muafaka ili uwekezaji uweze kufanyika kwa sababu wananchi wanahitaji huduma bora zaidi na eneo hilo linatosha kwa matumizi yote ya elimu pamoja na huduma za afya.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel amesema kuwa Serikali imewekeza fedha nyingi kwenye sekta ya afya hasa kwenye miundombinu, teknolojia ya afya pamoja na kwenye wataalamu, kwani kwa sasa kuna wataalamu wa kutosha

# Wadau sekta ya afya wakabidhi vitendea kazi vya thamani ya milioni 800 kwa serikali

**Na. Abdulwaheed Madenge**
**DODOMA**

Serikali kupitia Wizara ya Afya imepokea vitendea kazi vyenye thamani ya Milioni 800 kutoka kwa wadau wa CDC kupitia THPS kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI na Kifua Kikuu katika Mkoa wa Tanga.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amepokea vitendea kazi hivyo Februari 23, 2024 Mkoani Tanga ambavyo ni pikipiki 50, friji 72, Centrifuges 56, Compyuta 50, UPS 50 na printa 50 ambavyo vitendea kazi hivyo vitaimarisha huduma za Afya katika Mkoa huo.

Wakati akipokea vitendea kazi hivyo Waziri Ummy amewataka wote watakaokabidhiwa vifaa hivyo kuvitumia Kama ilivyo elekezwa ikiwa ni pamoja na kuwafikia wateja wanaoishi katika mazingira magumu na mbali na vituo vya kutolea huduma za Afya ili kuwafikishia huduma.

“Lakini pia tunaamini kwamba mtaongeza idadi ya huduma mkoba ‘outreach services’, kuwafikia wateja walio katika mazingira hatarishi ya kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI na kuwapatia huduma za kinga zikiwemo kinga dawa na kusafirisha sampuli kwa ajili ya kupima wingi wa Virusi vya UKIMWI.” Amesema Waziri Ummy.

Pia, amewataka kutunza vifaa hivyo na kuvifanyia matengenezo ya mara kwa mara ili viweze kudumu kwa muda mrefu na kutimiza lengo la kudhibiti UKIMWI na VVU ambapo ametoa onyo kwa yeyote atakae fanya kinyume na maelekezo hayo kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

Pia, Waziri Ummy Mwalimu ameyataka Mashirika yote ya kiraia yanayofanya kazi katika Sekta ya Afya angalau watenge kiasi kisichopungua asilimia 10 kwa ajili ya kuajiri watumishi wa Afya katika vituo vya kutoa huduma za Afya ngazi ya msingi.

“Tunaposema kupambana na masuala ya UKIMWI lakini kuna upungufu wa wauguzi, hakuna madaktari, hakuna watu wa maabara, hakuna wafamasia, angalau muajiri wauguzi wawili na watumishi wengine wa mikataba.” Amesema Waziri Ummy.





# Watoto zaidi ya milioni 8 nchini kupatiwa chanjo ya surua rubella

**Na. Said Nyaoza**
**DODOMA**

Serikali kupitia Wizara ya Afya imezindua kampeni ya Kitaifa ya Chanjo ya Surua Rubella ambapo kwa nchi nzima wanatarajia kuwafikia watoto 8,908,810 wenye umri chini ya miaka mitano.

Hayo yamebainishwa  Jijini Dodoma na Kaimu Mkurugenzi Idara ya Kinga kutoka Wizara ya Afya, Dkt. Tumaini Haonga akimuwakilisha Waziri wa Afya, Mhe. Ummy Mwalimu katika uzinduzi wa kampeni ya chanjo Kitaifa Februari 15, 2024 katika maeneo mbalimbali nchini na inatarajiwa kumalizika Jumapili Februari 18, 2024.

Dkt. Haonga amesema kuwa lengo la kampeni hii ni kuhakikisha wanazuia kuenea kwa ugonjwa surua na rubella pamoja na kuongeza kinga kwa walengwa.

Dkt. Haonga amesisitiza usimamizi wa chanjo hiyo kutokana na umuhimu wake kwani inaongeza kinga kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Ameongeza kuwa zaidi ya vituo 7,373 katika maeneo mbalimbali nchini vimetengwa kwa ajili ya kuhakikisha wanatoa Huduma hiyo kikamilifu ili kuweza kufikia lengo walliojiwekea..

Hata hivyo amewataka Wakuu wa Mikoa,Wilaya na Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuhakikisha wanasimamia kikamilifu zoezi kuwapatia chanjo watoto wenye umri kuanzia miezi tisa mpaka 59 (chini ya miaka mitano)

"Niwaombe wazazi kuitumia fursa hii kuwapeleka watoto wao waweze kupatiwa chanjo kwani ni muhimu kwa watoto kupata chanjo hiyo,"ametoa wito Dkt. Haonga.

Dkt. Haonga amesema wamepata mrejesho tangu kuanza kwa chanjo kwa zoezi hilo katika maeneo mbalimbali wazazi wamejitokeza kwa wingi na wanaendelea kujitokeza ili kulinda afya za watoto wao.



# Madaktari 9 wakutwa na hatia kufuatia uvunjifu wa maadili ya kitaaluma

**Na. Emmanuel Malegi**
**DAR ES SALAAM**

Baraza la Madaktari Tanganyika limewatia hatiani na kuwapa adhabu madaktari Tisa kwa makosa ya ukiukwaji wa kanuni za maadili na utendaji wa kitaaluma na kutoa maamuzi dhidi ya wanataaluma hao kupitia Kikao cha Baraza la Madaktari Tanganyika kilichokaa kati ya tarehe 22 hadi 26 Januari 2024 lililosikiliza jumla ya mashauri Tisa.

Hayo yamebainishwa Februari 9, 2024 na Mwenyekiti Baraza la Madaktari Tanganyika Prof. David Ngassapa akiwa anazungumza na waandishi wa habari kuhusu mashauri ya Kitaaluma yaliyowasilishwa mbele ya Baraza hilo Januari 2024.

Miongoni mwa adhabu zilizotolewa ni pamoja na kufutiwa usajili, kufungiwa leseni ya kutoa huduma kwa muda kati ya miezi sita hadi wa miaka Miwili, kupewa onyo au karipio kali na pia walielekezwa kwenda kwenye mafunzo ya weledi, maadili ya kitaaluma na huduma kwa mteja ya Wizara ya Afya kwa muda wa miezi sita kwa gharama zao.

Aidha, Mwenyekiti Prof. ngassapa amesema Baraza linatoa rai kwa wanataaluma wote nchini kuzingatia Kanuni na maadili ya kitaaluma za mwaka 2005 na kufuata miongozo ya utoaji huduma kwa lengo la kulinda Afya ya Mgonjwa.

Baraza limebaini pia baada ya mapitio ya mashauri mbalimbali kuwa maeneo mengi ya misingi ya maadaili ya kitaaluma yameonekana kutokutiliwa maanani na wanataaluma kwenye kutoa huduma za Afya kwa wagonjwa.

"Hivyo, Baraza linaelekeza kuzingatiwa kwa misingi ya maadili wakati wa kutoa huduma ikiwemo kujaza fomu za ridhaa ya huduma (informed Consent) kwa mgonjwa, kumuelimisha mgonjwa madhara yanayoweza kujitokeza wakati wa matibabu na kuwa kushindwa kufuata hayo, watakuwa wameenda kinyume na Sheria ya Udaktari, Udaktari wa Meno na Afya Shirikishi Sura Na. 152 pamoja na kanuni zake.

# JE UNA MAONI, USHAURI, PONGEZI AU KERO NA MALALAMIKO KUHUSU HUDUMA ZA AFYA?

**Usijali sasa tumekufikia, tuma taarifa yako kwa njia ya ujumbe wa kawaida au Whatsapp au kwa baruapepe afyamaoni@afya.go.tz**



**+255 763 050 000**

**#TunaboreshaAfya**
**#MtuniAfya**
**#Afyanimtaji**




**Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**WIZARA YA AFYA, TANZANIA, TOLEO LA MWEZI FEBRUARI, 2024**